JARIDA LA

# SAUTI YA JIJI

DAR ES SALAAM

ISSN 0856-9711 | TOLEO NA. 13 | DISEMBA, 2021



## "KUELEKEA MIAKA 60 YA UHURU, JIJI TUPO VIZURI"

### UONGOZI:
KASI YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA NDANI YA JIJI

### AFYA KINGA:
MATUMIZI SAHIHI YA MPANGILIO WA VYAKULA

### MICHEZO:
KUIBUA VIPAJI MASHULENI

### ELIMU:
ONGEZEKO LA UFAULU NA UJENZI WA MADARASA

### LIFAHAMU JIJI:
MABADILIKO YA TABIA YA NCHI

#JijiTupoVizuri

# JARIDA LA SAUTI YA JIJI

**BODI YA WAHARIRI**

**MWENYEKITI**

BI. TABU F. SHAIBU
*Mhariri*

**WAJUMBE**

NEEMA NJAU
*Mhariri Msaidizi*

HASHIMU JUMBE
*Mwandishi*

JUDITH MSUYA
*Mwandishi*

AMANZI KIMONJO
*Mwandishi*

ROSETHA GANGE
*Mwandishi*

**MSANIFU WA JARIDA**

FEROOZ KILLAH

*Jarida hili hutolewa na;*
Kitengo cha Habari, Uhusiano na Mawasiliano
S.L.P 20950, DAR ES SALAAM
OFISI YA MKURUGENZI
1 MTAA WA MISSION
SIMU: 2128800
2128805
WEBSITE: www.dcc.go.tz
EMAIL:administration@dcc.go.tz






## YALIYOMO

**UK- 01**
*Kasi nzuri ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam*

**UK- 05**
*Halmashauri ya Jiji yajenga Vyumba 178 vya Madarasa*

**UK- 07**
*Utoaji wa Elimu Maalum*

**UK- 08**
*Michezo Mashuleni*

**UK- 11**
*Mabadiliko ya Tabia ya Nchi*

**UK- 15**
*Afya Kinga*

**UK- 19**
*Halmashauri yatoa Mkopo wa Shilingi Bilioni Mbili (2) kwa Wanawake,Vijana na watu wenye ulemavu*

# KASI NZURI YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI CHAMA CHA MAPINDUZI NDANI YA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM KWA KIPINDI CHA JANUARI HADI JUNI 2021

Na Tabu Shaibu:

## Utangulizi;

Malengo ni njia imara ili kutimiza mipango ya Taifa katika ngazi zote za kiutawala kwa nia ya kujenga na kuimarisha uchumi stahiki wa nchi hiyo, Tanzania kupitia chama cha mapinduzi (CCM) inatumia Ilani kama dira inayowaongoza kutekeleza mipango iliyojiwekea 2020-2025.

Kwa kiasi kikubwa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam imeweza kutekeleza ilani hii kama ibara na vifungu vya ilani hiyo ilivyoelekeza kutokana na miradi mbalimbali ya maendeleo kutekelezwa sambamba na kuendana na kauli ya Rais wa Jamuhuri wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan ya "KAZI IENDELEE...." katika nyanja mbalimbali ikiwemo elimu, afya na ustawi wa jamii, mifugo na uvuvi, mipango miji na ardhi pamoja na maendeleo ya jamii.

Utoaji wa huduma za Elimu

## Elimu ya Awali.

Jiji la Dar es salaam limeandikisha wanafunzi wa rika lengwa wa darasa la awali na uandikishwaji umeongezeka kwa asilimia kubwa yaani kutoka 100% 2020 na kufikia 125% Juni 2021. Wanafunzi walioandikishwa ni 12,926 kati yao wasichana 6,521 wakati wavulana wakiwa 6,365 kwa mwaka 2021, Ujenzi wa jumla ya vyumba 5 vya madarasa ya awali vimejengwa kwa gharama ya shilingi Milioni 75 huku matundu 15 ya vyoo yaliyogharimu kiasi cha shilingi Milioni 16.5 ikiwa ni fedha za ruzuku (EP4R) yamejengwa katika shule za Kiyombo, Bombambili, Buyuni II na Yongwe.

Jumla ya madawati 100 yamenunuliwa na kusambazwa kwenye shule zenye upungufu ikiwemo shule ya Zanaki na Kisutu ambapo kiasi cha shilingi Milioni 15 zimetumika ikiwa ni fedha za mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam na wadau wa maendeleo.Hii ni wazi kuwa Halmashauri inatekeleza ibara ya 80 (b) inayosema "kuhakikisha kuwa kila shule ya msingi inatoa elimu ya awali kwa ufanisi katika mazingira na miundombinu iliyoboreshwa."



## Elimu ya Msingi.

Katika Ibara ya 80 (a) inayosema "kujenga na kukarabati miundombinu ya elimu Pamoja na kuhifadhi na kuendeleza mazingira ya shule hizo," Halmashauri ya Jiji la Da r es salaam imeweza kutekeleza mpango huo kwani idadi ya wanafunzi 31,359 ikiwa wasichana 16,211 na wavulana 15,148 wameandikishwa darasa la kwanza kwa mwaka 2021 hii ikiwa ni utekelezwaji wa waraka Na.3 wa mwaka 2016 'Elimu bila malipo'.
Sambamba na hilo idadi ya wanafunzi wanaoendelea na elimu ya sekondari (kidato cha kwanza) imeongezeka kutoka asilimia 98% mwaka 2019 na kufikia asilimia 100% mwaka 2021 huku ufaulu wa wanafunzi waliohitimu darasa la Nne umeongezeka kutoka asilimia 97% mwaka 2019 hadi asilimia 100% mwaka 2020.

Vilevile, ujenzi wa vyumba vya madarasa 62 na ofisi 2 za walimu katika shule ya msingi Mnazi Mmoja na Gulukakwalala uliyoghalimu shilingi Milioni 943 umetekelezwa kwa kipindi cha January hadi Juni 2021 ikiwa shilingi Milioni 508 zikiwa ni fedha kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam na shilingi Milioni 435 zikiwa ni fedha za ruzuku kutoka serikali kuu (EP4R).





Shule ya Msingi Gulukakwalala

Sambamba na hilo kiasi cha shilingi Milioni 164.7 zimetumika katika ujenzi wa matundu 161 ya vyoo katika shule za Msingi kwa kipindi cha January hadi Juni 2021 ambapo matundu 84 ya vyoo yenye thamani ya shillingi Milioni 80 ikiwa ni fedha kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri na wadau mbalimbali wa maendeleo(SOS)yamekamilika huku matundu 77 ya vyoo yenye thamani ya shilingi Milioni 84.7 ikiwa ni fedha za ruzuku kutoka Serikali kuu(EP4R) ujenzi unaendelea.

Aidha, Halmashauri imeendelea kuboresha miundombinu katika shule za msingi kwani kiasi cha shilingi Milioni 318.9 kutoka mapato ya ndani zimetumika kuboresha miundombinu hiyo ambapo shilingi Milioni 160 zimetumika katika ununuzi wa madawati 866 kwa shule zenye upungufu huku shilingi Milioni 158.9 zimetumika kukarabati vyumba 8 vya madarasa.

## Elimu ya Sekondari

Halmashauri ya jiji la Dar es salaam imejitahidi kujenga na kukarabati miundombinu ya elimu pamoja na kuhifadhi mazingira ya shule hizo ili kuinua kiwango cha taaluma katika shule za Sekondari.

Ibara ya 80 ya Ilani ya uchaguzi ya chama cha Mapinduzi (CCM) inayotaka kuimarisha ubora wa elimu katika ngazi zote kwa kuzingatia falsafa ya kujitegemea yenye kuendana na mazingira ya nchi yetu, hususani elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi imetekelezwa kwa kiasi kikubwa kwani uandikishwaji wa wanafunzi katika shule za sekondari za serikali umeongezeka kutoka 26,000 mwaka 2020 mpaka 26,447 kufikia June 2021.

Ujenzi wa vyumba vya madarasa 250 vya msambao katika shuke za sekondari na uanzishwaji wa shule mpya 10 unaendelea na kugharimu kiasi cha shilingi Bilioni 2.4 na mpaka kufikia Juni 2021 vyumba vya madarasa 136 vilikuwa vimekamilika na kuanza kutumiwa,na kwa baadhi ya shule ujenzi bado unaendelea.

Katika kuinua kiwango cha taaluma katika shule na kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani vyumba vya madarasa 100 vya ghorofa vimejengwa katika shule za Sekondari na kugharimu kiasi cha Shilingi Milioni 604 na mpaka kufikia June 2021 madarasa 42 yalikuwa yanaendelea kujengwa katika shule 5 na pia ujenzi umekamilika kwa baadhi ya shule hivyo kupunguza tatizo la msongamono wa watoto darasani.

Katika kipindi cha Januari-June 2021 halmashauri ya jiji la Dar es salaam iliwapa jumla ya walimu 452 mafunzo mtambuka.Walimu 120 walipata mafunzo ya scout wakati walimu 120 pia walipata mafunzo ya unasihi.Hali kadhalika walimu 212 walipata mafunzo ya PREMS.Mafunzo haya yote kwa walimu yaligharimu kiasi cha shilingi Milioni 18. Huu ni utekelezaji wa Ibara ya 80 ya Ilani ya Uchaguzi inayotaka kuimarisha ubora wa elimu .

Shule mpya 2 za sekondari zimeanzishwa katika kipindi cha mwezi Jan-June 2021ambapo ujenzi wake unaendelea na upo katika hatua ya ukamilishaji. Sambamba na hilo madawati 555 yamenunuliwa na kusambazwa katika shule mbalimbali zilizokuwa na upungufu mkubwa.Ujenzi wa shule Pamoja na ununuzi wa madawati umegharimu kiasi cha shilingi Milioni 687.7. Katika kuhakikisha wanafunzi wanaondokana na adha ya kupanga foleni kwa muda mrefu wakisubiri kwenda kujisaidia na kukosa baadhi ya masomo, Halmashauri ya jiji la Dar es salaam pia ujenga matundu 60 ya vyoo katika shule za sekondari zilizokuwa na upungufu na mpaka kufikia mwezi Juni 2021 ujenzi ulikuwa umekamilika na kugharimu kiasi cha shilingi Milioni 180.





Katika kutambua kwamba Ulimwengu tulionao hivi sasa ni ulimwengu wa Sayansi na Teknolojia na katika kuendana na zama tulizonazo hivi sasa, zama za Sayansi na Teknolojia, Halmashauri ya jiji la Dar es salaam inafanya jitihada za kuimarisha ufundishaji, ujifunzaji na utumiaji wa TEHAMA shuleni katika shule 102 za sekondari kwa kununua kompyuta 200.Mpaka kufikia mwezi Juni 2021 kompyuta 12 zimekwisha nunuliwa na kugharimu kiasi cha shilingi Milioni 14.4 na vifaa hivi vinaendelea kutumiwa na wanafunzi.Kama inavyojulikana michezo ni sehemu muhimu sana katika jamii kwa sababu michezo sio tu inatoa burudani kwa jamii baada kazi na kukuza mahusiano mazuri baina ya watu na watu,michezo hujenga afya ya mwili na akili,hujenga ukakamavu na pia michezo hujenga nidhamu.Katika kutambua hili Halmashauri ya jiji la Dar es salaam imejitahidi kuimarisha na kuhamasisha Sanaa na michezo shuleni na kujenga viwanja 100.Pia imenunua vifaa vya michezo na kuvisambaza katika shule za sekondari na kusaidia michezo ya Umiseta katika ngazi zote kuweza kufanyika kiurahisi na kugharimu kiasi cha Shilingi Milioni 118.8.



TEHAMA Mashuleni

## Huduma za Afya

Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025, Ibara ya 83 inaitaka Serikali kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya na siha bora ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za ujenzi wa Taifa na kuboresha maisha yao. Kipengele (a) cha Ibara hiyo kinataka kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto na kuzitoa bila malipo ili kupunguza vifo vya akina Mama wajawazito na Watoto wenye umri chini ya miaka mitano(5). Katika Halmashauri ya jiji la Dar es salaam Ibara hii imetekelezwa wa kiwango kikubwa kwani Wajawazito wanaotarajia kujifungua walifikiwa na akina mama wapatao 30,744 walijifungua kutoka vituo 105 vya serikali na binafsi vinavyotoa huduma ya mama na mtoto ambapo haya yote yaligharimu kiasi cha shilingi Milioni 51.8.

Ibara ya 83(b) Serikali inataka kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba,vifaa saidizi na vitendanishi kulingana na mahitaji katika ngazi zote za utoaji wa huduma za afya nchini. Halmashauri ya jiji la Dar es salaam imelitekeleza hili kikamilifu katika kipindi cha Januarl hadi Juni 2021 na kununua dawa,vifaa tiba,vifaa saidizi na vitendanishi na makasha yapatayo 10,840 yalinunuliwa na kugharimu kiasi cha shilingi Bilioni 1.3 na yatasambazwa katika kila robo ya mwaka kwenye vituo vya kutolea huduma za afya.

Aidha katika Ibara hiyohiyo kifungu (d) kinasisitiza kujenga na kuimarisha vituo vya kutolea huduma za afya ili viweze kutoa huduma bora Zaidi kwa wananchi,vipaumbele vitawekwa katika ujenzi wa vituo vya afya na ukamilishwaji wa maboma kwa kuzingatia uwiano wa kijiografia,idadi ya watu na wingi wa magonjwa.Katika kutekeleza hili Halmashauri ya jiji la Dar es salaam ina mkakati wa kumalizia ujenzi wa majengo ya Hospitali ya Wilaya, kumalizia ujenzi wa kituo cha Afya Mzinga na Guluka kwalala na kujenga nyumba za watumishi 6.Mpaka kufika Juni 2021 Halmashauri ya jiji la Dar es salaam ilikuwa inamalizia ujenzi na kuanza kutoa huduma za Afya kwa wananchi katika Zahanati ya Luhanga mradi huu kugharimu kiasi cha shilingi milioni 100.Pia bajeti ya ukamilishwaji wa Zahanati hii na Kituo cha Guluka kwalala upo katika bajeti ya 2021/2022.

Kifungu (m) cha Ibara ya 83 ya Ilani ya Uchaguzi kinataka kuhamasisha jamii umuhimu wa matumizi ya vyandarua vilivyoweka dawa na upuliziaji wa viatilifu ukoko katika kuta za nyumba na Halmashauri ya jiji la Dar es salaam imejitahidi kutoa elimu nyumba kwa nyumba ili kuongeza ufahamu wa matumizi ya vyandarua katika kila kata.Hili limefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwani Wananchi wapatao 1,256,213 ambayo ni sawa na 76.2% ya wananchi wote wa jiji la Dar es salaam wanatumia vyandarua.

Mbali na hayo Ibara ya 83(o) inalenga kutoa elimu na kuhamasisha wananchi kupambana na magonjwa ya kuambukiza (UVIKO 19, VVU na UKIMWI ,TB, Homa ya Ini na Malaria) na yasiyoambukizwa (Shinikizo la damu, kansa na figo) Pamoja na kununua na kusambaza dawa zake na kuhamasisha upimaji wake ili wananchi waweze kutambua hali zao na kuchukua hatua stahiki.Katika kutekeleza hili serikali,mashirika,Taasisi na wadau mbalimbali wa afya wamekuwa wakijitahidi sana kupambana kadiri inavyowezekana kupunguza makali ya magonjwa haya kwa kutoa elimu kwa jamii jinsi ya kujikinga na jinsi ya kupunguza uwezekano wa kusambaa Zaidi.Kwa upande wa Halmashauri ya jiji la Dar es salaam kwa kipindi cha mwezi January-June 2021 imejitahidi kutoa elimu katika shule 45 za kata zote 36 juu ya kujikinga na UVIKO -19.

Ili kuondokana na adha ya wagonjwa kukaa kwenye foleni kwa muda mrefu na kurahisisha kazi kwa watoa huduma za afya,Serikali imeimarisha matumizi ya TEHAMA kwenye vituo vya afya.Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020/2025 Ibara ya 83(q) inasema,Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa huduma za afya ikiwemo tiba mtandao,mafunzo,utawala,usimamizi wa fedha,dawa na bidhaa zote za dawa Pamoja na uboreshaji wa ukusanyaji na matumizi ya takwimu za afya katika hospitali,hospitali za Wilaya,vituo vya afya na zahanati.Katika kutekeleza hili,Halmashauri ya jiji la Dar es salaam iliweka mikakati ya kuweka mfumo wa Gothomis kwenye vituo vipya vitakavyojengwa na kukarabati mifumo iliyopo ili ifanye kazi kwa ufanisi mpango ambao umefanikiwa kwa kiasi kikubwa kwani kufikia Juni 2021 vituo 24 kati ya 29 vimepatiwa kompyuta kwa ajili ya matumizi ya TEHAMA na kugharimu kiasi cha Shilingi Milioni 50.5.Vilevile vituo vipya 5 vitapata huduma ya TEHAMA katika bajeti ya 2021/2022.

Taifa lolote duniani lazima liwe imara katika utoaji wa huduma za afya kinyume na hapo raia wake hawataweza kufanya kazi ipasavyo kwani magonjwa ya mara kwa mara ambayo hayatibiwi kwa wakati yanaweza kuathiri utendaji wao hivyo kuathiri pia maendeleo ya nchi.Katika kuliangalia hili Kifungu (u) cha Ibara ya 83 ya Ilani ya Uchaguzi kinalenga kuimarisha huduma za afya ya mama na mtoto katika vituo vyote vya kutolea huduma za afya na kuzifanya rafiki kwa wanawake, wanaume na vijana ikiwemo kutoa huduma ya msingi ya dharura ya afya ya uzazi na mtoto na huduma tembezi ya mkoba.Katika hili Halmashauri ya jiji la Dar es salaam iliazimia kuwa na huduma tembezi kila baada ya miezi sita katika vituo vya kutolea huduma na kufanya ziara za mkoba kila robo mwaka ili kuhakikisha huduma inayotolewa ni stahiki kwa akina mama.Kwa kushirikiana na wadau wa vituo binafsi, katika kipindi cha mwezi Januari-June huduma ya mkoba imefanyika katika vituo vya serikali 20 na vituo 15 vya binafsi na kugharimu kiasi cha shilingi milioni 2.1.

Sambamba na kifungu hicho juu,kifungu (y) cha Ibara hiyohiyo kinalenga kuimrisha ushirikiano na sekta binafsi katika utoaji wa huduma za afya. Halmashauri ya jiji la Dar es salaam iliazimia kuwa na vikao vya kila robo mwaka na wamiliki wa vituo vya afya binafsi ili kuboresha huduma.Katika kipindi cha mwezi January-Juni 2021 kliniki 9 za kibingwa na zahanati 11 za watu binafsi zilisajiliwa ili kutoa huduma kwa wananchi.

Kutoka na Ibara ya 93 ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM inayohamasisha kuimarisha huduma za ustawi kwa Watoto, Halmashauri ya Jiji la DSM imeweza kuimarisha elimu ya malezi kewa wanafamilia pamoja na uwepo wa malezi mbadala ili malezi ya Watoto yapatikane kwene familia kwani jumla ya mashauri ya ndoa kuhusiana na matunzo ya Watoto 1082 yalipokelewa na watotot kupatiwa huduma stahiki.

Kamati 29 za ulinzi na usalama wa mwanamke na mtoto zimeundwa katika ngazi ya Kata na moja ya Halmashauri ili kuhakikisha afua zote za ulinzi na usalama wa wanawake na Watoto zinatekelezwa lengo likiwa ni kuimarisha ulinzi na usalama wa Watoto pamoja na kulinda maadili chanya ya Taifa.

Jumla ya vituo 94 vya malezi ya watoto wadogo vimesajiliwa ngazi ya Halmashauri pamoja na walezi 10 kutoka katika kata waliopaata mafunzo wameweza kutoa huduma kikamilifu kwa Watoto waliokosa makazi ya kifamilia lengo likiwa ni kuwawezesha Watoto kupata malezi stahiki kutoka kwa wataalamu.

Chama cha Mapinduzi (CCM) kinaamini kwamba: “Binadamu wote ni sawa na kila mtu anastahili heshima ya kutambuliwa na kuthaminiwa utu wake”. Kwa imani hii , katika kipindi cha Januuary hadi Juni 2021 Halmashauri ya Jiji la DSM imeweza kutekeleza hilo kwani jumla ya watu 1528 wenye ulemavu wametambuliwa ikiwa watu 67 ni wenye ulemavu wa Ngozi (Albinism), viziwi 157 wasioona 192, walemavu wa viungo 935 pamoja na walemavu wa akili 200.

Utoaji wa huduma za matibabu kwa wazee umeimarishwa kwani jumala ya shilingi milioni tano na laki mbili(5,2000,000/=) zimetolewa hivyo kusaidia wazee takrbani 5144 kupata huduma za matibabu kwa msamaha pia kupitia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam jumla ya wazee 1443 wamepatiwa kadi za mfuko wa afya ya jamii iCHF

Mapambano Dhidi ya Magonjwa ya Mlipuko ikiwemo Korona.
Magonjwa ya mlipuko ni yale magonjwa ambayo hutokea wakati wowote bila kutarajia.Ikumbukwe kuwa mwezi March mwaka 2020 ugonjwa wa Korona uliibuka hapa Tanzania na kusababisha taharuki kubwa miongoni mwetu.Lakini Raisi wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania aliyekuwepo wakati huo hayati John Pombe Magufuli alikabiliana nao na kuweza kuudhibiti,na mpaka sasa Raisi aliopo madarakani Mh.Samia Suluhu Hassan ameudhibiti kikabilifu kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo kuhamasisha wananchi kupata chanjo ili kuepuka uwezekana wa kuathirika Zaidi na ugonjwa huo.Hii inatokana na Ibara ya 84 ya Ilani ya Uchaguzi ya chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020/2025 inayosema, Nchi inakuwa na utayari wakati wote wa kuzuia,kudhibiti na kukabiliana na majanga na magonjwa ya mlipuko kwa kushirikiana na wadau wengine.Katika kuweka msisitizo kifungu cha (f) cha Ibara hii kinaagiza kujenga na kuimarisha maabara za uchunguzi wa magonjwa ya mlipuko,vituo vya kisasa vya kuwatenga wahisiwa (Isolation centres) na kutoa tiba kwa wagonjwa.Kwa upande wake Halmashauri ya jiji la Dar es salaam iliweka mkakati wa kumalizia na kuweka vifaa katika jengo la magonjwa ya mlipuko Kipawa.Katika hili jiji limefanikiwa kuweka miundombinu ya jengo katika kupambanana mlipuko wa magonjwa katika kata ya Kipawa na kazi ya ukamilishaji wa jengo hilo bado unaendelea ambapo gharama za mradi huu mpaka kufikia Juni 2021 ilikuwa kiasi cha shilingi Milioni 205.

Maendeleo ya Jamii

Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam imetekeleza Ilani ya chama cha mapinduzi kama ibara ya 26 (c) ilivyosema "kuwezesha vijana ,wanawake na makundi mengine ya wajasiriamali kujiajiri kwa kuwapatia mafunzo na stadi za ujasiriamali pamoja na usimamizi wa shughuli za kiuchumi na kuwezesha kurasimisha shughuli zao ifikapo mwaka 2025" Halmashauri imetekeleza jambo hili kwa kufanikisha kutoa mafunzo kwa vikundi 192 vya vijana na wanawake juu ya usimamizi wa fedha na uanzishaji wa miradi.Miongoni mwao wanawake 100 na vijana 92, hii ni kutokana na mpango wa ilani ya chama ya kuendelea kutoa mafunzo zaidi kwa vijana ili vijana na wanawake waweze kujiajiri wenyewe hivyo kupunguza tatizo la ajira.

Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam sambamba na kuwezesha vijana na wanawake pia imeweza kubuni na kuhakikisha mikakati ya kutoa elimu kwa vijana juu ya ujasiriamali, elimu rika, afya ya uzazi na stadi za Maisha na jumla ya vijana 750 wamenufaika na wamepatiwa mafunzo hayo ikiwa ni utekelezaji wa Ibara ya 26 (g) ya ilani ya chama cha CCM inayosema "kubuni na kutekeleza mikakati ya kuhakikisha kuwa elimu ya ujasiriamali inayotolewa na wadau mbalimbali ikiwemo sekta binafsi na asasi za kiraia ina ubora unaokidhi mahitaji ya vijana na walengwa wengine".

Vilevile, Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam imeweza kufanikisha kutoa mikopo isiyo na riba kwa vikundi 269 katika kata 36 iliyogharimu shilingi Bilioni 3.2 ambapo shilingi Bilioni 1.3 ni mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya Vijana Pamoja na shilingi Bilioni 1.9 imetolewa kwa vikundi vya Wananawake hii ni kuonesha kwamba Ilani inatekelezwa kama Ibara ya 32 (s) iliyoeleza kuwa "kuhakikisha kwamba Halmashauri zote nchini zinaendelea kutenga fedha kwa ajili ya mfuko wa maendeleo ya wanawake ,Vijana na watu wenye ulemavu kwa mujibu wa sheria ili kuwezesha vijana na makundi mengine katika jamii zetu kupata mikopo isiyo na riba"

Mapambano Dhidi ya VVU/UKIMWI na Madawa ya Kulevya.

Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam imeweza kuendelea kuratibu shughuli za kupunguza kasi ya maambukizi dhidi ya VVU na UKIMWI mapambano dhidi ya Magonjwa haya imeghalimu jumla ya shilingi Milioni 47.5 ikiwa ni utekelezaji wa ilani ya chama cha mapinduzi ibara ya 88 (f) isemayo "kuimarisha ushiriki wa jamii kuwawezesha kushiriki katika kupiga, kutekeleza na kufuatilia afua za kijamii katika mazingira yao kwenye mapambano dhidi ya UKIMWI".

Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam imeweza kutoa elimu ya madhara ya matumizi ya dawa za kulevya jumla ya vijana 455 ikiwa wanawake 103 na wanaume 352 ambao wamepatiwa elimu kwa kushirikiana na shirika la MKIKUTE sambamba na ibara ya 245(a) ya ilani ya chama isemayo "kulinda mafanikio yaliyopatikana katika vita dhidi ya dawa ya kulevya kwa kuendelea kuibua na kutekelez mikakati ya kupambana na kudhibiti biashara na utumizi wa dawa za kulevya".

Kilimo,ushirika na umwagiliaji.

Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam imetumia ghalama ya shilingi laki 6,655,000. Kuwezesha ununuzi wa vifaa vya kisayansi na kuweka (istallation) ya vifaa kwenye maabara ndogo ya kilimo katika kitua cha kata cha rasilimali kilimo kinyamwezi pia sambamba na hilo Halmashauri ya Jiji imefanya malipo ya jumla ya shilingi Milioni 47,579,000 ikiwa na mchanganuo ufuatayo malipo ya ununuzi wa vifaa kuoitia mzabuni malipo ya fundi kwa ajili ya kujenga mnara na mtandao wa kusambaza maji shambani Pamoja na contingency yamefanyika kisima kimekamilika na kimeanza kutumika ghalama iliyotumika ni shilingi Milioni 15.3 Pia malipo ya fundi cert.02 & 03 yamefanyika ulikua unaghalama ya shilingi Milioni 2.4 na malipo ya unuuzi wa vifaa kupitia mzabuni malipo ya fundi cert. 01 pamoja na malipo ya contingency yamefanyika na umetumia ghalama ya shilingi Milioni 29.7 hapa bado ujenzi unaendelea.

Pia,Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam imeweza kufanya uwezeshaji na utoaji wa mafunzo ya kilimo katika sehemu mbalimbali ikiwa jumla ya shilingi Milioni 12.6 ikiwa mafunzo ya rejea kuhusu matumizi sahihi ya viuatilifu kwa maafisa ugani umefanyika ikiwa ni utekelezaji wa agizo la waziri wa kilimo Mhe. Adolf Mkenda kufuta siku ya wakulima NANENANE 2021 Mnamo tarehe 10.02.2021 kwa ajili ya kuimarisha huduma za ugani mafunzo haya yalitumia shilingi Laki 9.405.000, sambamba na hilio pia Halmashauri ilitumia shilingi Laki 3. kwa kuwawezesha maafisa ugani 2 kushiriki mafunzo ya viutilifu TPRI Arusha na kwa upande wa wanafunzi Halmashauri imewezesha mafunzo ya siku 2 kwa wanafunzi wa shule ya msingi Zanaki kuhusu kilimo bora cha mboga kwa kutumia teknolojia ya kilimo mjini yamefanyika na shilingi Laki 2.0 zimetumika.

Mifugo na Uvuvi.

Ibara ya 40(a) ya Ilani ya chama cha mapinduzi inasema "kuendeleza na kuimarisha huduma za ugani katika ngazi ya kata na vijiji kwa kuhakikisha kuwa kila mfugaji anafikiwa na huduma za ugani" kwa kutekeleza hili Halmashuri ya Jiji la Dar es salaam imeendeleza ujenzi wa machinjio na ununuzi wa vitendea kazi ya machinjio ya vingnguti ulioghalimu Milioni 756.3 ikiwa shilingi milioni 662.4 fedha zilizotolewa kwa ajili ya kukamilisha ujenzi na shilingi milioni 89.9 ni fedha zilizotumika kwa ajili ya ununuzi wa vitendea kazi vya machinjio ya kisasa ya Vingunguti.





Juu ya hayo, pia ukarabati wa kituo cha mafunzo ya mifugo Msongola (Mvuti) yamefanyika Pamoja na kujenga mabucha eneo la machinjio ya vingunguti umefanyika na kughalimu jumla ya shilingi Milioni 47.6 imetumika ikiwa Milioni 37.4 ni kwa ajili ya ukarabati wa darasa na nyumba ya mtumishi sambamba na shilingi Milioni 10.2 fedha hizi zilitumika katika ujenzi wa mabucha maeneo ya Vingunguti.





# HALMASHAURI YA JIJI LA DSM YAJENGA VYUMBA 178 VYA MADARASA YA SEKONDARI, YATEKELEZA AGIZO LA WAZIRI MKUU



**Na: Hashim Jumbe**

**T**AREHE 18 Disemba, 2020 akiwa kwenye ziara ya ukaguzi wa vyumba vya madarasa Shule ya Sekondari Buhongwa Mkoani Mwanza, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa aliziagiza Halmashauri zote nchini zihakikishe zoezi la ujenzi wa vyumba vya madarasa liwe endelevu kwa sababu idadi ya wanafunzi walioandikishwa na wanaotarajiwa kujiunga na kidato cha kwanza inafahamika. "Ni lazima Mtoto wa Kitanzania aliyefaulu aende Sekondari, jukumu la Halmashauri ni kuhakikisha inajenga vyumba vyakutosha vya madarasa. Ifikapo Februari 28, 2021 ujenzi wa vyumba vya madarasa uwe umekamilika na kuwawezesha wanafunzi wa kidato cha kwanza kuingia darasani," Alisema Mhe.-Majaliwa. Itakumbukwa kuwa Serikali ya Awamu ya Tano (5) iliyokuwa ikiongozwa na aliyekuwa Rais wa wakati huo, Hayati Rais John Pombe Magufuli ilipitisha waraka wa Elimu Namba 6 wa Mwaka 2015 kuhusu utekelezaji wa elimu bure kwa shule za msingi na sekondari, Waraka huo ulioanza kutekelezwa Januari 2016 umechangia kuinua sekta ya elimu na kuongeza idadi ya wanafunzi wanaoandikishwa darasa la kwanza na wanaoingia kidato cha kwanza kwani mpango huo umesaidia kuongeza ufaulu

Ongezeko hilo la wanafunzi limepelekea Serikali kuongeza kasi kubwa ya uboreshaji wa miundombinu katika mashule kwa kuweka mazingira bora ya kujifunzia na kufundishia sambamba na kuajiri walimu ili kuendana na ongezeko hilo.

Aidha, kwa upande wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam umeweza kutekeleza agizo la Waziri Mkuu kwa mafanikio makubwa, kwa kujenga Shule mpya Mbili (02) za Sekondari ambazo ni Kipunguni yenye vyumba vya madarasa kumi (10) na Bwawani vyumba vya madarasa Tisa (09), pia imejenga vyumba vya madarasa ya ghorofa Ishirini na Nane (28) katika Shule za Sekondari Gerezani, Mnazi Mmoja, Kasulu, Kimanga, Migombani na Msimbazi, vyumba vingine 131 vya madarasa ya msambao vimejengwa katika Shule nyengine tofauti za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na kufanya jumla ya vyumba vya madarasa vilivyojengwa kufikia 178.

"Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam tulikuwa na idadi kubwa ya wanafunzi waliofaulu kuingia kidato cha kwanza kwa mwaka huu 2021 idadi ya wanafunzi 28,400 walichaguliwa na kufanya kuwe na ongezeko la wanafunzi, ongezeko hilo la ufaulu lilipelekea tuwe na upungufu wa vyumba vya madarasa 178, hivyo katika kuhakikisha wanafunzi wote wanaingia darasani, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam tumetumia Shilingi Bilioni 3.3 kutoka katika fedha za makusanyo yetu ya ndani na kujenga vyumba vya madarasa 178, hivyo wanafunzi wote waliofaulu wamepata vyumba vya kusomea" Jumanne Kiangio Shauri Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Lakini pia, ujenzi wa vyumba hivyo vya madarasa sambamba na uanzishwaji wa shule mpya mbili (02) za Sekondari kwa Kata za Kipunguni na Kiwalani ambazo hazikuwa na Shule za Sekondari ni moja kati ya mipango ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam katika kukabiliana na ongezeko hilo la wanafunzi lililotokana pia na kuanza kutolewa elimu bila malipo, ujenzi wa shule hizo umekuwa na faida kubwa kwa wakazi wa maeneo hayo.

"Ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari Kipunguni una faida kwetu Wananchi wa Kipunguni, kwani utasaidia Wazazi kuwafuatilia watoto wao kwa ukaribu, kujua kama wanafika shuleni au hawafiki, hivyo itasaidia kupunguza utoro mashuleni, lakini pia itapunguza gharama za nauli ya kila Siku, na pia itasaidia watoto kutokuamka alfajiri kuwahi usafiri kwenda shule za mbali, sasa hivi watoto wataamka muda wa kawaida na watapata muda wa kupumzika na kujisomea, kwa hiyo ujio wa Sekondari ya Kipunguni utaongeza pia ufaulu kwa watoto" Mhe. Stephen Mushi, Diwani wa Kata ya Vingunguti

Pamoja na jitihada za ujenzi wa vyumba vya madarasa, lakini pia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeendelea kufanya uboreshaji wa miundombinu katika mashule kwa kukarabati madawati yenye uchakavu na kutengeneza madawati mapya 6,551 ili kukidhi upungufu uliopo wa madawati, uhitaji wa madawati hayo umechagizwa pia na ongezeko la wanafunzi "Kwenye baadhi madarasa yalikuwa hayana madawati, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam tumetoa fedha kwa ajili ya kutengeneza madawati 6,551 na pia tumekarabati madawati zaidi ya 10,000 ambayo yalikuwa yameharibika, hivyo pamoja na kujenga vyumba vya madarasa lakini pia tumehakikisha hakuna mtoto atakayekosa kiti cha kukalia" Jumanne Shauri Mkurugenzi wa Jiji

Katika hatua nyengine, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeweza kujenga matundu 60 ya vyoo katika shule ya Sekondari Ari ambayo imejengwa matundu ya vyoo Kumi na Tano (15) Sekondari ya Chanika matundu ya vyoo Kumi na Tano (15) Sekondari mpya ya Kipunguni matundu ya vyoo Kumi na Tano (15) na Sekondari ya Bwawani matundu ya vyoo Kumi na Tano (15)

Sambamba na maboresho hayo, lakini Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwa kipindi cha Januari hadi Machi, 2021 imeweza kupokea fedha ya ruzuku kutoka Serikali Kuu kwa ajili ya ujenzi wa Mabweni katika shule za Sekondari ya Azania mabweni mawili na mabweni mawili Sekondari ya Mkera iliyopo Kata ya Msongola kwa lengo la kukabiliana na changamoto iliyokuwa inawakabili wanafunzi wanaotokea maeneo ya mbali. "Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam tumepokea fedha kiasi cha Shilingi Milioni 320 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mawili kwa Shule ya Azania na mabweni mawili kwa ajili ya ujenzi wa mabweni mengine mawili ya shule ya sekondari Mkera, kukamilika kwa ujenzi wa mabweni haya kutasaidia wanafunzi 160 wa Mkera na 160 wa Azania kuweza kulala shuleni, hivyo kutaongeza ufaulu kwa watoto wetu" Jumanne Shauri, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji



Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Ndugu Jumanne K. Shauri alipofanya ukaguzi kuangalia ujenzi wa vyumba vya madarasa Shule ya Sekondari Kinyerezi Annex sambamba na Mbunge wa Jimbo la Segerea Mhe. Bonnah Kamoli



Ujenzi wa shule mpya ya Sekondari Bwawani iliyopo kata ya Kiwalani



Mstahiki Meya wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam Mhe. Omary Kumbilamoto akikagua ujenzi wa Shule mpya ya Sekondari Kipunguni

# UTOAJI WA ELIMU MAALUM SHULE ZA JIJI LA DAR ES SALAAM .

**Na;Rosetha Gange**

Katika maisha yetu ya kila siku tumekuwa tukisikia watu wakisema "Elimu maalumu" lakini katika hali ya kawaida mtu anaweza asielewe moja kwa moja nini tafsiri ya kauli hiyo au maneno haya. Pia tunaweza kukutana na kauli kama watu wenye mahitaji maalumu, pia kwa haraka haraka tunaweza tusielewe maana yake ni nini.

Mtaalam wa masuala ya Elimu kwa watu wenye mahitaji maalum na Mkuu wa Kitengo cha Elimu maalumu kutoka Halmashauri ya jiji la Dar es salaam Bw.Swalehe Msechu anasema kuwa,Elimu maalumu ni elimu inayotolewa kwa watoto au watu wenye mahitaji maalumu, wakati Watu wenye mahitaji maalumu ni watu wenye changamoto mbalimbali ambao pia wapo katika makundi mbalimbali kama ulemavu wa akili au ufahamu,ulemavu wa macho,ulemavu wa viungo,Viziwi ambao kuna viziwi wasioona na viziwi wanaoona na wengine wengi.

Bw.Msechu anaongeza kuwa,Watoto wenye mahitaji maalumu wanaweza kutoka katika mazingira mbalimbali au mazingira tofauti tofauti mfano kuna watoto wanaotoka kwenye mazingira ya wafugaji wa kuhama hama,watoto yatima yaani waliofiwa na wazazi wao,watoto wa maskini (wale wasioweza kupata mahitaji yao ya muhimu),wawindaji wanaohama hama kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine,watoto wenye changamoto za kiafya, mfano wale wenye magonjwa ya kudumu ambayo huchukua muda mrefu sana kupona,watoto ambao ni mahabusu wa muda mrefu,watoto wenye magonjwa adimu ambayo hayawaruhusu kuchangamana na watoto wengine hivyo kuwalazimu kujitenga au kukaa peke yao,watoto wa mitaani na watoto wanaoshuhudia ugomvi wa kifamilia mara kwa mara (watoto wenye matatizo ya kisaikolojia kutokana na mazingira wanayotoka).

Anafafanua kuwa sio kila mtu au mtoto mwenye mahitaji maalumu ni mlemavu lakini watu wote wenye ulemavu wanaingia katika kundi la watu wenye mahitaji maalumu.Na ulemavu upo wa aina nyingi kama ulemavu wa akili, usonji, viziwi (wasioona na wanaoona), ulemavu wa viungo na watu wenye ualbino, ulemavu wa wasioona (hawawezi kuona maandishi ya kawaida, anaweza kuwa haoni kabisa au akawa na uoni hafifu).

Anaongeza kuwa watoto wenye ulemavu wa akili wamegawanyika katika makundi manne;

1. Watoto wenye ulemavu wa akili mkubwa sana.
2. Watoto wenye ulemavu wa akili mkubwa.
3. Watoto wenye ulemavu wa akili wa wastani.
4. Watoto wenye ulemavu wa akili mdogo.

Watoto wenye ulemavu wa akili mkubwa sana kwa kawaida ni wale ambao ulemavu wao wa akili upo katika kiwango cha juu.Yaani hakuna kitu ambacho wao kama wao wanaweza kukifanya bila usaidizi wa watu wengine,hivyo watoto wa namna hii huduma ya elimu haiwezi kuwafikia.Watoto wa namna hii wanahitaji huduma za kitabibu zaidi hivyo kumlazimu kuwepo hospitalini wakati wote.



Kulia Afisa Elimu Maalum wa Jiji la Dar es salaam Bw. Swalehe Msechu akiwaelezea jambo kwa Lugha ya Alama walimu na Wanafunzi wa Shule ya Sekondari Benjamini Mkapa.

Elimu maalumu huwafikia watoto wenye ulemavu wa akili namba tatu na namba nne ambapo wale wenye ulemavu wa akili wa wastani, wao husoma kwa hatua tatu yaani hatua ya kwanza, hatua ya pili na hatua ya tatu.Lakini anaweza akasoma asimalize hatua zote tatu kutokana na changamoto ya ulemavu alionao.Na kama atapita au kufanikiwa kumaliza hatua zote tatu, atakuwa amefuzu kuingia darasa la kwanza katika shule za kawaida. Watoto wenye ulemavu mdogo hawa huwa na changamoto ndogo ndogo ambazo sio kikwazo sana kwa wao kujifunza au kupata elimu.Mfano anaweza akaanza darasa la kwanza na akaendelea mpaka kufika elimu ya juu.

Viziwi ni watu ambao hawawezi kupokea mawimbi ya sauti.Nao wamegawanyika katika makundi ya wanaoona na wale ambao hawaoni.Viziwi wasioona na wale ambao hawaoni wala kusikia na hawa hutumia mawasiliano yao kwa njia ya kugusa mfano anaweza kumpapasa au kumgusa mtu kujua ni mwanamke au mwanaume, anaweza kupapasa maandishi kujua ni nini kimeandikwa (hutumia maandishi ya nukta nundu), anaweza pia kushika vitu mbalimbali ili kuweza kuvitambua kuwa ni vitu gani.

Viziwi wanaoona ni watu ambao wanaona lakini hawasikii,na watu wa namna hii hutumia ishara kama lugha yao ya mawasiliano.

Usonji.Watoto wenye usonji ni watoto walioathirika kwenye milango ya fahamu,yaani wana changamoto ya ufahamu na sio ulemavu wa akili.Kuathirika kwa watoto hawa katika milango ya fahamu kunawapelekea kuwa na kasoro katika maeneo matatu yaani kwenye mahusiano ya kijamii,mawasiliano na masuala ya utambuzi.Kwenye mawasiliano wao hawana lugha maalumu ambayo huitumia kuwasiliana lakini hutumia ishara zaidi kuliko alama.

Halmashauri ya jiji la Dar es salaam, Idara ya Elimu Msingi na Idara ya Elimu Sekondari kitengo cha Elimu Maalumu kimefanikiwa sana katika utekelezaji wa sera ya Elimu kwa wote bila kuangalia watoto au watu hao wanakabiliana na changamoto zipi. Mkuu wa kitengo cha Elimu maalumu Bw.Swalehe Msechu anawatoa wasiwasi na anaendelea kujibu baadhi ya hoja ambazo zimekuwa zikiwaumiza vichwa baadhi ya wanajamii kiasi cha kuchelea au kusita kuwafichua watoto wenye mahitaji maalumu au wenye changamoto mbalimbali na kuwapeleka shule.

> Kumekuwa na tabia ya wanajamii wengi kuwaficha watoto wenye mahitaji maalumu hasa watoto wenye ulemavu. Je, kitengo cha elimu maalumu kinafanya nini au kina mpango gani katika kuwafichua watoto wote waliofichwa ili waweze kupelekwa shule na kupata haki yao ya msingi ya elimu?

Bw.Msechu anasema kuwa, ni kweli kulikuwa na changamoto ya wanajamii kutowapeleka watoto shule lakini kwa sana hali hiyo imepungua kwa sababu hapo awali walikuwa hawajui kama kuna shule za watoto wenye mahitaji maalum, walikuwa hawajui kama watoto hawa wanaweza kupata elimu, walikuwa hawajui watoto hawa wanaweza kuwa msaada kwao pia walikuwa hawajui kama watoto hawa wanaweza kuja kujitegemea wenyewe na sio tegemezi.

Halmashauri ya jiji la Dar es salaam, Idara ya Elimu Msingi na Idara ya elimu Sekondari kitengo cha elimu maalumu wanajitahidi sana kuhamasisha jamii kupitia vyombo vya habari kama televisheni, magazeti, redio na majarida mbalimbali. Pia kupitia matangazo ya nyumba kwa nyumba na kupita kwenye mitaa yote,kufanya makongamano mbalimbali ya kuhamasisha na kuelimisha wanajamii,kufanya vikao na walimu wakuu wote wa shule na kuwaelimisha ni nafasi ipi mtoto anaweza kuipata kwa kupata elimu maalumu.Pia wanapofanya vikao mashuleni,huwaita wanafunzi na kuwaeleza nini maana ya elimu maalumu na mtoto mwenye mahitaji maalumu anasoma vipi na endapo atasoma nini faida yake.Hii hufanya wanafunzi hawa kuwa mabalozi wazuri wanapokwenda majumbani kwao, na kuwaeleza wenzao na hata wazazi wao.Pia hii husaidia endapo wataona watoto wenye ulemavu wamefungiwa ndani kuhoji na kuwaelimisha wazazi na watoto hao kuwa wao pia wanaweza kupata elimu kama watoto wengine.

Pia katika kata zote 36 za Halmashauri ya jiji la Dar es salaam, kila kata wamejitahidi kufungua shule ambazo zinatoa elimu jumuishi kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalumu.Yaani katika kila shule kuna kitengo cha elimu maalumu.

Anaongeza kuwa hapo zamani elimu maalumu ilikuwa inapatikana katika maeneo ya mijini tu, lakini yeye kama mkuu wa Idara ya Elimu maalumu amejitahidi kuwafuata wananchi kwa kuwapelekea huduma mpaka kwenye maeneo walipo na sio wao kuifuata huduma. Mfano kwa maeneo ya pembezoni mwa mji, mpaka sasa huduma ya Elimu maalumu imekwishawafikia wakazi wa maeneo ya Chanika, Msongola, Majohe, Kinyerezi na Bonyokwa.

Kwa upande wa vyoo kwa ajili ya watu wenye ulemavu Msechu anasema kuwa anapozungumzia miundombinu ya watu wenye mahitaji maalumu ni pamoja na uwepo wa vyoo kwa ajili ya watu wenye changamoto mbalimbali.Anasema kuwa hapo nyuma Afisa Elimu Msingi aliyestaafu Mama Elizabeth Thomas aliwahi kuanzisha kampeni maalumu iliyoitwa 'Binti makini mwamvuli wangu stara' ambapo kilitengenezwa choo cha mtoto wa kike. Choo hicho kilikuwa ni cha mtoto mwenye ulemavu na shule zote 18 zinazotoa elimu maalumu zina vyoo maalumu kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalumu.Pia hata zile shule jumuishi zina choo cha mtoto mwenye mahitaji maalumu.Anaongeza kuwa hivi karibuni amepata mfadhili ambaye ni Alliance Club aliyetoa ahadi ya kutatua changamoto ya vyoo katika shule zote za jiji la Dar es salaam na katika vyoo hivyo ni lazima viwepo vyoo kwa ajili ya watoto wenye mahitaji maalumu.

Kwa ujumla jamii inabidi ielewe kwamba watoto wenye mahitaji maalumu nao ni watu kama walivyo wanajamii wengine, hivyo wana haki ya kupata elimu kama ilivyo kwa wengine.Pia Serikali, Mashirika binafsi na wadau wengine wa elimu kuendelee kuielimisha jamii kuepuka unyanyapaa kwa watu wenye changamoto mbalimbali na kuwaita majina yasiofaa kwani kufanya hivyo kunasababisha familia zenye watoto wenye changamoto hizo kuendelea kuwaficha hivyo kusababisha wao kukosa haki yao ya kupata elimu.

> "watoto wengi wenye mahitaji maalumu wanaofanya mitihani ya kumaliza elimu ya msingi wanafaulu kwa kiwango cha juu



# MICHEZO, UTAMADUNI NA MAENDELEO YA ELIMU KATIKA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM.

**Na: Judith Msuya**

Michezo ni sehemu ya maisha ya kila mwanadamu,usipopenda kushiriki uwanjaniutaishabikia,michexo hujenga mwili,huburudisha, hukuza uwezo wa kufikiri na pia hudumisha undugu.Taaluma ya michezo ni pande mbili za shilingi wanafunzi hupenda michezo kwa kuimarisha upande wao wa taaluma. Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeweka juhudi za kuibua kuibua michezo katika shule zote za halmashauri kwa madhumuni ya kutengeneza baadae iliyo bora kwa wanafunz katika taaluma zao na hata vipaji vyao ili viwakwamue katika hali ya maisha ,nafasi ya vipaji katika jamii ni kubwa sana kwani kupitia mashuleni wanafunzi hugundua hasa wapi na nini wanapenda na kutambua vipaji walivyonavyo. Shule za sekondari na msingi zimekua zikishiriki katika michezo ndani ya shule na hata nje ya shule kulingana na ratiba ya serikali kuwepo kwa Umoja wa michezo Sekondari Tanzania (UMISETA) na Umoja wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) kwa madhumuni ya kuibua wanariadha,waruka kamba, warusha tufe,wachezaji wa mpira wa miguu,mpira wa mikono kwa wanawake, ngoma na vipajin vingine vingi ili kuimarisha afya na taaluma zao mashuleni.

Kwa upande wa mashindano ya Umoja wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) na Mashindano ya Umoja wa Michezo Sekondari Tanzania (UMISETA) yanayokutanisha timu tano kutoka katika Halmashauri za mkoa wa Dar es Salaam ambazo ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, Manispaa ya Kinondoni, manispaa ya Temeke, Manispaa ya Ubungo pamoja na Manispaa ya Kigamboni,Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam wamekua vinara wakutwaa ubingwa kwa Mkoa wa Dar es Salaam miaka mitano(5) mfululizo huku wakitoa wachezaji wengi zaidi kwenda timu ya Mkoa wa Dar es Salaam ambao huwa hushiriki katika ngazi ya Taifa.
Licha ya mashindano hayo ya UMISETA na UMITASHUMTA inabidi tusisahau utamaduni wetu kwani michezo ya kiutamaduni ni soko zuri la ajira kwa vijana wa Kitanzania.
Wahenga walisema Mkataa kwao Mtumwa kwani lazima tulinde tamaduni zetu ambapo tunaposema neno Utamaduni hii inamaanisha ni jumla ya namna ya maisha wanaoishi kikundi Fulani Au Jamii katika eneo Fulani la Kijografia, hii ni sambamba na namna ya kula, namna ya kuvaa, namna ya kuongea, na michezo mbalimbali kama ngoma za asili na muziki . Katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam shule za Msingi zimekua maarufu katika kudumisha michezo na ngoma za asili (fani za ndani) kwa lengo la kuenzi utamaduni wa Mtanzania na Afrika kwa ujumla.

"Namshukuru Mungu kwani wanafunzi wangu niloanza nao michezo ya ngoma za asili katika shule ya Msingi Lumumba hawakuishia hapo wameweza kuunda kikundi chao cha LUMUMBA THIETRE na kuhakikisha wanacheza ngoma hizo kiheshima na kiutamaduni zaidi hivyo nikipata mialiko Mingi nje ya nchi huwa naenda nao". Alisema Mwl. Dyuto.

Kwa upande mwingine Mtazamo sahihi ni kuwa na mfumo bora wa kusimamia michezo ya kiutamaduni ambao mfumo bora utalazimu vyombo husika kama serikali na wadau wote washiriki kikamilifu katika kuwezesha kufikia malengo kwani mwalimu Dyuto Komba hakuishia hapo katika safari yake ya kukuza vipaji na kuendeleza utamaduni wa Mtanzania ambapo hata baada ya kuhamishwa shule ya msingi Lumumba na kupelekwa shule ya msingi Kiwalani alipambana kuwabadilisha wanafunzi wa shule hiyo na kuhakikisha wanapenda michezo na wanafanya vizuri katika masomo yao pia. Vilevile, Mwl.Komba aliweza kuteka hisia na mawazo ya wanafunzi wa shule ya kiwalani na kuanzisha kikund cha sanaa za asili kiitwacho UMOJA GROUP katika shule ya Msingi Kiwalani.

Wahenga walisema,Mchumia juani hulia kivulini , hii ikiwa na maana kuwa pamoja na ugumu huo wa kuanzisha sanaa za Kiutamaduni kwa lengo la kuwawezesha vijana kupata ajira na kutosahau Tamaduni zao pia Mwl.Komba aliweza kupata mafanikio katika ngazi ya elimu na kijamii kwani wanafunzi walikua rafiki na waliweza kupata matunda yafuatayo;

Mwl. Komba alifanikiwa kwa kiasi kikubwa kupunguza utoro kwa wanafunzi wa shule ya msingi kiwalani kwani baada ya kuanzisha kikundi cha ngoma wanafunzi wengi walifurahia kuwaona wenzao wanavyocheza na kuimba hivyo kuwalazimu kufika shuleni kila siku.

Kwa upande mwingine Mtazamo sahihi ni kuwa na mfumo bora wa kusimamia michezo ya kiutamaduni ambao mfumo bora utalazimu vyombo husika kama serikali na wadau wote washiriki kikamilifu katika kuwezesha kufikia malengo kwani mwalimu Dyuto Komba hakuishia hapo katika safari yake ya kukuza vipaji na kuendeleza utamaduni wa Mtanzania ambapo hata baada ya kuhamishwa shule ya msingi Lumumba na kupelekwa shule ya msingi Kiwalani alipambana kuwabadilisha wanafunzi wa shule hiyo na kuhakikisha wanapenda michezo na wanafanya vizuri katika masomo yao pia. Vilevile, Mwl.Komba aliweza kuteka hisia na mawazo ya wanafunzi wa shule ya kiwalani na kuanzisha kikund cha sanaa za asili kiitwacho UMOJA GROUP katika shule ya Msingi Kiwalani.

Wahenga walisema,Mchumia juani hulia kivulini , hii ikiwa na maana kuwa pamoja na ugumu huo wa kuanzisha sanaa za Kiutamaduni kwa lengo la kuwawezesha vijana kupata ajira na kutosahau Tamaduni zao pia Mwl.Komba aliweza kupata mafanikio katika ngazi ya elimu na kijamii kwani wanafunzi walikua rafiki na waliweza kupata matunda yafuatayo;

Mwl. Komba alifanikiwa kwa kiasi kikubwa kupunguza utoro kwa wanafunzi wa shule ya msingi kiwalani kwani baada ya kuanzisha kikundi cha ngoma wanafunzi wengi walifurahia kuwaona wenzao wanavyocheza na kuimba hivyo kuwalazimu kufika shuleni kila siku.



*"Haikua raisi kwangu kuweza kuanzisha michezo ya kiutamaduni katika shule ya msingi Kiwalani kwani baada ya kufika shuleni hapo mazingira ya shule yalikua sio rafiki kwangu hivyo niliweka jitihada kubwa sana za kuweza kufanya mazingira kuwa rafiki kwangu ili kuwashawishi wanafunzi na wazazi wao kukubali na kushiriki ngoma za Kitamaduni. Licha ya hivyo jitihada zangu ziliweza kufanikiwa na kuanzisha kikundi cha UMOJA GROUP katika shule ya msingi Kiwalani".*

# #Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa akagua ujenzi wa Machinjio ya Kisasa - Vingunguti











**Naibu Meya wa Jiji la Dar es Salaam Mhe Saady Khimji (Aliyevaa suti) akiwa katika ziara Kata ya kitunda katika Zahanati ya Kitunda na kusikiliza changamoto mbalimbali ambazo zinaikabili zahanati hiyo.**







# HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM LAJIPANGA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIA NCHI.



KINGO ZA FUKWE YA OCEAN ROAD

Na: Rosetha Gange

Mabadiliko ya tabia nchi ni hali ya kuongezeka kwa hewa ukaa angani ambayo inasababisha kufyonza joto na kulikuza zaidi,hivyo joto linavyoshuka kwenye uso wa dunia linakuwa na ukali Zaidi ya lilivyokuwa hapo awali.

Hewa ukaa ambayo kwa jina jingine hujulikana kama jopogesi ni moja ya gesi hatari ambazo zipo angani. Gesi hizo zipo katika aina kuu tatu nazo ni gesi ya Carbondiaxide, gesi ya Methani na gesi ya Nitrodioxide ambazo inaaminika ni gesi hatari zaidi katika anga.

Katika kipindi cha Zaidi ya mwezi mmoja sasa hapa kwetu Tanzania tumekuwa tukishuhudia ongezeko la vipindi vikubwa vya jua wakati wa mchana na kuongezeka kwa joto kwa nyakati za mchana hata usiku. Hali hii imekuwa ikileta maswali mengi miongoni mwa wanajamii juu ya sababu hasa ya kutokea kwa hali hii inayoleta adha kubwa sio tu kwa binadamu hata Wanyama pia wameathirika sana ya mabadiliko haya ya tabia nchi kwani mbali tu ya kukauka kwa vyanzo vya maji kunakopelekea watu kupata huduma ya maji kwa shida, Wanyama pia hufa kutokana na kiu ya maji ya muda mrefu.

Wataalamu wa mambo ya mazingira wamekuwa wakijitahidi kubuni njia mbalimbali za jinsi ya kukabiliana na Mabadiliko haya kwani mbali na kuwa na athari za kimazingira na kusababisha athari kwa mtu mmoja mmoja ,mabadiliko hayo pia huwa na athari za kiuchumi pia.

Bi.Neema Sita ambaye ni Afisa Mazingira kutoka Halmashauri ya jiji la Dar es salaam anaeleza sababu za kitaalam zinazosababisha mabadiliko ya tabia nchi kutokea na njia wanazozitumia kukabiliana na mabadiliko haya ili yasiweze kuleta athari Zaidi kwa jamii.

Anasema kuwa Mabadiliko ya tabia nchi husababishwa na sababu kuu mbili nazo ni 'Kazi za kibinadamu' na 'Majanga ya asili.'Kwenye sababu ya kwanza ambayo ni kazi za kibinadamu kunatokea pale maendeleo ya viwanda yanapokuwa makubwa kwani kwani shughuli za uzalishaji viwandani zikizidi ule moshi wa viwandani husababisha kwenda angani na kusababisha uchafuzi wa hewa na kubadilika kwa hali ya hewa kwa ujumla. Pia kazi za kibinadamu kama ukataji wa miti,uchimbaji wa madini na utupaji wa taka ovyo pia husababisha mabadiliko ya tabia nchi. Mfano kuna wachimbaji wa madini ambao hutumia milipuko kupasua miamba hivyo kusababisha hewa chafu kwenda angani na kusababisha uchafuzi wa hali ya hewa.Pia ukataji wa miti ovyo huchangia mabadiliko ya tabia nchi kwa sababu uwepo wa miti huchangia mvua kunyesha kwa wingi hivyo ukataji wa miti huchangia vipindi virefu vya jua na ukame katika sehemu fulani.

Majanga ya asili huchangia mabadiliko ya tabia nchi pale ambapo kutatokea ulipukaji wa volkano na kutokea kwa mioto ya asili.

Mara kwa mara tumekuwa tukisikia maeneo mbalimbali hasa misitu ikiwaka moto bila mtu yeyote kuanzisha mioto hiyo na kusababisha athari kubwa sana kwa mazingira.Mfano mwaka 2019 vyombo vya habari vya kimataifa viliripoti msitu wa Amazon nchini Brazil kuwaka moto na kusababisha athari kubwa kwa wakazi wa nchi hiyo ikiwemo matatizo ya kupumua hasa kwa watoto.Pia moto huo ulisambaa mpaka kufika katika msitu wa bonde la Kongo na kuhatarisha upatikanaji wa mvua katika maeneo yanayopakana na msitu huo kwani msitu wa bonde la Kongo unatajwa kuchangia kusafisha hewa chafu ya Kaboni kwa kiasi kikubwa.

Kutokana na kuongezeka kwa mabadiliko ya tabia nchi Bi.Neema anasema kuwa,wao kama Idara ya Mazingira na udhibiti wa taka ngumu kutoka Halmashauri ya jiji la Dar es salaam wanatumia njia mbalimbali katika kukabiliana na tatizo hili ili lisiweze kuleta madhara zaidi kwa wanajamii.

Upandaji wa miti. Halmashauri ya jiji la Dar es salaam kupitia kitengo cha mazingira kimejitahidi kupanda miti katika sehemu mbalimbali zilizo wazi na katika maeneo ya shule ili kuongeza ufyonzaji wa hewa ya ukaa kutoka angani na kuleta hewa safi.

Ujenzi wa kingo za bahari ya Hindi. Mojawapo ya athari za mabadiliko ya tabia nchi ni kupungua kwa kina cha bahari na mmomonyoko wa kingo za bahari.Hivyo Halmashauri ya jiji la Dar es salaam imeanzisha mradi wa ujenzi wa kingo za bahari katika eneo la Ocean road ili kuweza kuzuia mmomonyoko huo ambao unaweza kusababisha madhara makubwa kwa wakazi wa jiji la Dar es salaam.

Ujenzi wa kingo za mito, madaraja na mifereji.Halmashauri ya jiji la Dar es salaam imefanikiwa kujenga kingo za mto Msimbazi, ujenzi wa kingo za mto mpogo uliopo maeneo ya Ilala,ujenzi wa mfereni wa maji taka katika mtaa wa Liwiti kuelekea bonde la mto Msimbazi,ujenzi wa mfereji maeneo ya Buguruni Malapa n.k.Hii yote ni katika kuhakikisha endapo mafuriko yanatokea yasiweze kuathiri jamii inayoishi maeneo jirani na mito au mifereji hiyo.

Vilevile kuna mradi wa Dar green ambao unaendelea kupitia mradi wa DMDP ambapo mradi huu unajishughulisha na upandaji wa miti pamoja na ujenzi wa madaraja.Mradi wa upandaji miti utasaidia sio tu kupendezesha mazingira bali kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Aidha kuna mpango wa kuanzisha mradi wa kuendeleza kingo za mto Msimbazi ambao unatarajiwa kuwapunguzia wananchi adha ya kuingiliwa na maji katika maeneo yao hasa barabara na makazi yao, ambapo mara nyingi tumekuwa tukisikia vifo kutokea sababu ya mito kufurika.

Halmashauri ya jiji la Dar es salaam pia inatoa elimu kupitia magari ya matangazo juu ya jinsi ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwa kuzunguka katika maeneo mbalimbali ya jiji la Dar es salaam pia inatoa elimu kwa wanafunzi kwenye shule za msingi na Sekondari ya vyanzo vya mabadiliko ya tabia nchi na njia za kukabiliana na mabadiliko hayo.

Mradi wa kusambaza majiko mbanifu.Majiko haya yanasambazwa kwa lengo la kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi, badala ya watu kutumia majiko ya mkaa wanashauriwa kutumia majiko mbanifu ambayo hutumia mkaa unaotengenezwa kwa makaratasi na wataalamu wa mazingira wamethibitisha kuwa ni salama kwa afya za watumiaji na mazingira kwa ujumla.

Halmashauri ya jiji la Dar es salaam ina misitu miwili ambayo ni msitu wa Zingiziwa uliopo kata ya Zingiziwa na msitu wa nyuki uliopo kata ya Kinyerezi.Kazi kubwa ya misitu hii ni kuendeleza kasi ya kufyonza hewa ukaa iliopo angani na kuleta hewa safi.

Bi.Neema anatoa wito kwa jamii kutumia jitihada mbalimbali ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwani utunzaji wa mazingira sio jukumu la kiongozi tu bali ni wajibu wa kila mwananchi.Anaikumbusha jamii ule usemi usemao, 'Ukiyatunza mazingira yatakutunza, bali ukiyaharibu nayo yatakuharibu.'

Katika kupunguza athari mbalimbali zinazoweza kutokea katika kipindi hiki cha joto kali, wataalamu wengine wa Mazingira wanashauri kutotembea juani kwa muda mrefu na kunywa maji kwa wingi, kuacha maji kwenye vyombo vyanje ili ili kuzuia wadudu hatari kama nyoka kuingia ndani kutafuta maji. Pia jamii inashauriwa kufunga vizuri milango na madirisha ili kuzuia wadudu hatari kuingia ndani ya nyumba na kuleta madhara kwa familia.

Kwa ujumla Halmashauri ya jiji la Dar es salaam kwa kiwango kikubwa imejitahidi sana kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi kwakubuni miradi mbalimbali ambayo itasaidia kuyalinda mazingira na kuepuka athari zinazoweza kutokea kwa jamii.Pia jamii inaonyesha kuifanyia kazi elimu inayotolewa kwani tunashuhudia kampeni mbalimbali za utunzaji wa mazingira zikiendeshwa huko mitaani na vikundi mbalimbali vya kulinda mazingira vikianzishwa.

# MPANGO WA MAENDELEO

## KWA USTAWI WA TAIFA WA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO - 19



1961 - 2021

Jiji tupo vizuri, Kazi iendelee

**Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam tunakushukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa Mgao wa Fedha Tshs Bilioni 5.1 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa shule za Sekondari**



SHULE YA SEKONDARI MINAZI MIREFU



SHULE YA SEKONDARI MAGOLE



SHULE YA SEKONDARI KINYEREZI



SHULE YA SEKONDARI KEREZANGE

# #Utunzaji wa Mazingira ni Jukumu letu sote





Safisha - Pendezesha Jiji la Dar es Salaam

# BARAZA LA MADIWANI - 2021









# AFYA BORA NI KINGA

**Na Mwandishi wetu**

Afya bora ni hali ya ukamilifu kimwili, kiakili, kijamii na kutokuwepo kwa maradhi.

Afya ni nguzo na raslimali muhimu katika maendeleo ya mtu binafsi, familia na nchi katika kuleta maisha bora na kupunguza umaskini. Hivyo basi uwezeshaji wa jamii katika kushiriki na kupanga kisha kutekeleza juu ya suala hili ni jambo muhimu katika kuwaletea maendeleo.

Kwa muktadha huo Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, imeendelea kutoa kipaumbele katika huduma za afya zenye ubora na zinazowafikia wananchi ili kuleta ustawi wa maisha na afya zao.

Kupitia Idara ya Afya, Halimashauri ya Jiji la Dar es salaam imeweka nguvu katika sehemu hii kuhakikisha wakazi wake wanapata haki yao ya msingi ya huduma bora za afya.

Katika kufanikisha azma hiyo Halimashauri, inatekeleza mkakati kabambe wa Afya Kinga uliogawanywa katika katika maeneo mbalimbali ya msingi, ambayo ni;
(i)Afya na Usafi wa Mazingira (Sanitation and Hygiene).
(ii)Usalama na Ubora wa Chakula (Food Hygiene and Safety).
(iii) Afya na Usalama Mahala pa Kazi (Occupational Health and Safety).
(iv) Ufuatiliaji na Udhibiti wa Mlipuko wa Magonjwa(Disease Control and Surveillance).
(v) Usimamizi wa Sheria (Law Enforcement).
(vi) Utoaji Elimu ya Afya katika Jamii(Health Education).
Halimashauli inatekeleza mambo hayo kwa kuzingatia kanuni na sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2009.

**(i)AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA**

Hali ya Ujenzi wa Vyoo bora na sehemu za kunawa Mikono

Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam inatekeleza eneo hili kama ilivyoainishwa katika Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2009, kifungu cha 52 hadi cha133.

Shughuli kubwa zilizofanyika ni utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Afya na Usafi wa Mazingira ambayo ilizinduliwa na Rais wa Serikali ya awamu ya tano Dk. Jakaya Kikwete katika Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, mkoani Kilimanjaro mwaka 2013.

Lengo la kampeni hii ni kuhakikisha kila Kaya inakuwa na choo bora na inakitumia kwa usahihi.

Hii inaendana na usemi maarufu wa Usichukulie Poa Nyumba ni Choo.

Hilo linaenda sambamba na kuhakikisha kila kaya ina sehemu ya kunawia mikono, sabuni na maji tiririka, ili kujikinga na magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu, kuharisha, kuharisha damu,homa kali ya mapafu (Uviko-19), na maradhi mengine.

Takwimu za kuanzia Januari hadi Disemba mwaka 2020 zinaonyesha kuwa, katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, jumla ya kaya zenye vyoo zilikuwa ni asilimia 98.5% na kati ya hizo kaya zenye vyoo bora zilikuwa ni asilimia 97.09% ambapo kaya zisizokuwa na choo ni asilimia 1.15%.

Kaya zenye sehemu za kunawa mikono katika kipindi cha Januari hadi Disemba mwaka 2020 zilikuwa ni asilimia 69.13%.

Mabadiliko haya yamechochewa kwa kiasi kikubwa na utoaji wa elimu ya afya katika ngazi ya jamii na watu wengi kuzingatia maelekezo baada ya kuzuka kwa ugonjwa wa homa kali ya mapafu unaosababisha na virusi vya corona yaani Uviko-19.

Katika kufanikisha hili, Halimashauri imetekeleza mpango wa kuhamasisha jamii kupitia vyombo vya habari na vipindi katika redio.

Pia imetumia maadhimisho mbalimbali ya shughuli za afya kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa kuzingatia kanuni na taratibu za afya.

Viongozi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, nao wamekuwa chachu katika kutoa mchango mkubwa kuhamasiha jamii juu ya umuhimu wa ujenzi wa vyoo bora na sehemu za kunawia mikono.




*Mkuu wa Wilaya ya Ilala Mh. Ng'wilabuzu Ludigija, akihutubia wakati wa kuhitimisha Maadhimisho ya Siku ya Choo na Unawaji wa Mikono Duniani, iliyofanyika katika eneo la Ofisi ya Afisa Mtendaji Kata ya Buguruni,*

Katika hotuba yake hiyo, tMh. Ludigija amehamasisha kuhusu umuhimu wa choo bora na kutoa maelekezo kuhakikisha wananchi wanakuwa na vyoo hivyo.

Pia ameonya wananchi wanaotiririsha maji taka na kukaidi kufuata maelekezo na elimu waliyopewa wanachukuliwa hatua za kisheria.

Mfumo wa Maji Taka Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, ndiyo sura ya Mkoa wa Dar es Salaam, kutokana na kuwa na shughuli nyingi za kiuchumi, mwingilino wa watu na makazi.

Hivyo basi kwa mazingira hayo, uwepo wa mifumo bora ya maji taka ni muhimu Hata hivyo mfumo wa maji taka kwa katika Halmashauri hii bado unahangamoto hasa katikati ya Jiji.

Kwa kushirikiana na wadau wa ambao ni Malaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (DAWASA), wameendelea kulishughulikia kuboresha mifumo hii.

Aidha katika baadhi ya maeneo utajengwa mfumo wa majitaka (Sludge trament plant) pamoja na kuweka utaratibu mpya ambao majitaka yatanyonywa kwa kuzingatia ratiba baada ya ukaguzi kufanyika (Scheduled emptying).

Utaratibu huu umeanza kufanyika katika maeneo ambayo kiwango cha maji ardhini kipo juu sana (High water table area) ambayo ni Kiwalani, Kipawa, Liwiti, Tabata, Kimanga na Ukonga.

Pia katika Kata ya Vingunguti umeanza kufanyika utaratibu wa kuunganisha mfumo wa majitaka hadi kwenye mabwawa ya Vingunguti na kwenye mitaa ya Miembeni, Kata ya Mnyamani kwa kushirikiana na DAWASA.

Vyoo vya Umma Usimamizi wa vyoo vya umma 21 umeendelea kufanyika na wazabuni wamepewa kufanya kazi hiyo kwa niaba ya Halmashauri.

Hata hizvyo baadhi ya wazabuni walipewa zabuni ya kuendesha na kufanya ukarabati katika vyoo tisa (9) kabla ya kuanza.

Baada ya ukarabati timu ya wataalam kutoka Idara ya Ujenzi, Fedha na Afya ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaa, imefanya ukaguzi ili kuona kama ukarabati umefanyika kulingana na gharama za ujenzi zilizotolewa na Halmashauri (BQ).

Umakini ndio nyenzo katika vyoo vya umma ukizingatia usafi na utaratibu ili kukidhi hadhi ya vyoo kwa madhumuni ya kupiga vita magonjwa kwa afya ya mwanadamu.



*Timu ya wataalamu wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na DAWASA wakikagua maeneo ambayo mfumo wa majitaka utapita katika Mtaa wa Mjimpya, Kata ya Mnyamani.*

**(ii)Usalama na ubora wa Chakula z**

Kwa mujibu wa Sheria ya Afya ya Jamii ya Mwaka 2009 kifungu cha 134 hadi 148, Halimashauri ya Jiji la Dar es Salaam imekuwa ikitekeleza suala la Usalama na Ubora wa Chakula.

Lengo ni kuhakikisha chakula kinatunzwa, kuandalia na kuliwa katika ubora unaotakiwa ili kuzuia madhara na magonjwa mbalimbali kwa wananchi.

Katika kipindi cha mwaka 2020, Halimashauri imetoa elimu kwa baba na mama lishe zaidi ya 350 katika maeneo ya masoko na maeneo mengine.

Mafunzo hayo yalilenga kuwapa elimu baba na mama lishe juu ya shughuli zao, Uumuhimu wa mlp kamili na chakula salama.

Katika mafunzo hayo Halimashauri imetoa mafunzo kwa baba na mama lishe kutoka katika Soko la Kimataifa la Samaki Ferry, Mchikichini, Buguruni Tabata, Kigogofresh, Ilala, Kigogosambusa, Mnazimmoja, Kisutu na Gerezani ambapo wafanyabiashara hiyo ya chakula 338 wamenufaika.

Lengo ni kufikia Baba na Mama Lishe zaidi ya 2000 waliopo katika maeneo mbalimbali ya Halimashauri ya Jiji la Dar es salaam.

Kunawa mikono ni muhimu wakati wa kuandaa chakula Pia mlo kamili ni muhimu ukijumuisha nafaka, jamii ya kunde,mboga za majani, mafuta na matunda.





Wakaguzi kutoka Ujenzi, Afya na Fedha wakikagua hali ya ukarabati wa Choo cha Mkunguni, Lumumba na Karume.

**(iii) Ufuatiliaji na udhibiti wa Magonjwa ya Mlipuko na Magonjwa Mengine**

Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009, kifungu cha 19 hadi 34 kinatoa maelekezo namna ya kufuatilia na kushughulikia magonjwa ya mlipuko na magonjwa mengine.

Udhibiti na ufuatiliaji wa mwenendo wa magonjwa ya mlipuko ni jukumu mojawapo la msingi ambalo linabeba dhana nzima ya Kinga.
Lengo ni kuzuia mlipuko wa magonjwa na endpo utatokea basi ufuatilaji ufanyike.

**Malaria**

Kwa kutambua umuhimu wa kudhibiti ugonjwa wa malaria, Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam,imekuwa ikifanya jitihada kubwa katika kipindi cha mwaka 2018/2019.Takwimu za wagonjwa wa nje zinaonyesha asilimia 4.3 walikuwa na malaria na mwaka 2019/2020 wagonjwa walikuwa ni asilimia 3.8. Kwa muktadha huo inathibitisha maambukizi kupungua kwa asilimia o.5 kutokana na shughuli za udhibiti zinazofanyika.

Shughuli kubwa iliyofanyika ni ukamataji wa mbu wapevu ili kujua aina ya mbu waliopo katika maeneo maeneo mbalimbali na kuchukua hatua stahiki. Kwa kipindi hiki mbu wengi waliokamatwa walikuwa jamii ya Culicine ambao walikamatwa katika maeneo ya Kata za Kimanga, Kipunguni na Msongola. Katika kipindi cha mwaka 2018-2020 asilimia 0.7 ya mbu aina ya anopheline wamekamatwa na asilimia 78.5 ya Culicine wamekamatwa. Pia uangamizaji wa viluwiluwi umeendelea kufanyika katika kata 27 ambapo wahudumu 69 wamekuwa wakitoa huduma hiyo.





Pichani kushoto: Mbunge wa Jimbo la Ilala, Mussa Zungu (kushoto) akipata maelezo kutoka kwa Mratibu wa Malaria wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam wakati wa utekelezaji wa mbu kwa kupuliizia dawa ya viua dudu katika mazalia yao, Kata ya Jangwanina Pichani kulia: Mhudumu akiangalia uwepo wa Viluwiluwi katika mfereji.

**AFYA NA MAGONJWA YASIOAMBUKIZA**

Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, alitangaza maadui watatu wa Taifa. Maradhi, Ujinga na Umasikini.

Kutokana na hali hiyo, sera, mikakati, mipango na hata Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), vimeegemea katika kukabiliana na maadui hao. Hata hivyo maradhi yamekua adui mkubwa kwa maisha ya binadamu kutokana kupunguza nguvu kazi katika ngazi ya familia nahata taifa kwa ujumla.
Magonjwa yamegawanyika katika makundi matatu ambayo ni;

(i) Magonjwa yanayoambukiza

(ii) Magonjwa yasiyoambukiza.

(iii)Magonjwa ya mlipuko.

**MAGONJWA YASIYOAMBUKIZA:**

Katika kipindi cha hivi karibuni magonjwa haya yameshika nafasi ya juu katika magonjwa angamizi ulimwenguni.

Inaelezwa kuwa magonjwa haya yako katika nafasi kumi za juu ya magonjwa angamizi ulimwenguni.

Magonjwa hayo yasiyoambukiza ambayo yameingia katika nafasi kumi za juu ni pamoja na kuharisha, malaria,shinikizo la damu, homa ya mapafu, homa ya tumbo, magonjwa ya mfumo wa njia ya hewa, ajali,na upungufu wa damu.
Magonjwa yasioambukiza ni jumla ya magonjwa yanayohusisha zaidi mtindo wa maisha (life style), namna ya ulaji (eating style).
Pia kutokufanya mazoezi na hata kukaa bila kujishughulisha, hali inayothibitishwa na wataalamu kuwa ni chanzo kikubwa cha magonjwa kama ya kisukari, moyo na shikizo la damu.Ugonjwa kama kisukari chanzo chake kikubwa ni mtindo wa maisha katika ulaji hasa kula bila mpangilio hivyo kuwa na uzito mkubwa. Kutokufanya mazoezi kunasababisha mwili wa mwanadamu kunarundika mafuta mwilini hasa katika mishipa na kusababisha mishipa ya damu kusinyaa na kushindwa kuhimili kupitisha damu.Ulaji usiofaa unaambatana na aina mbali mbali za chakula kama vile wanga, protini na mafuta.

Mwili wa binadamu unahitaji kiwango stahiki cha makundi hayo ya chakula, kiasi kwamba kikizidi katika mwili na hujenga mkusanyiko wa chakula. Ikiwa mfumo wa chakula utashindwa kukitoa mwililini basi mwili unashindwa kufanyia kazi chakula hicho hivyo mtu hupata kitambi na uzito mkubwa hali inayofahamika kitaalamu kama BMI, ambapo mfumo wa kusaga chakula au mwili kupunguza sukari basi matokeo yake hutokea ugonjwa wa kisukari.

**Vyanzo vya magonjwa yasioambukiza viamegawanyika katika maeneo mbalimbali.**
Kuna magonjwa yanayotokana na mtindo wa chakula mfano Kisukari. Mengine yanatokana na mtindo wa maisha kama kula chumvi nyingi, kutokufanya zoezi na kuvuta sigara ambayo huchangia kusababisha ugonjwa wa moyo na shinikizo la damu.
Kuna magonjwa ambayo husabishwa kutokana na kutokufanya mazoezi , bila kujishughulisha, hivyo kusababisha mwili kushindwa kujiendesha wenyewe na mtu kushindwa kuudhibiti moyo.Uvutaji sigara wa mu mrefu husababisha mishipa inayopeleka damu katika mwili kukakamaa na kusinyaa.Ulaji wa chumvi nyingi kuliko mahitaji unasababisha maji mengi katika mzunguko wa damu kwa sababu kiwango cha chumvi lazima kiendane na maji.Kiwango cha a chumvi mwilini kikizidi na maji kuongezeka moyo utashindwa kusukuma damu hivyo mtu anaweza kupata shinikizo la damu.Vilevile, kuna baadhi ya aina za chakula ambazo zinaweza kuchangia kupata magonjwa ya saratani.

Mfano utumiaji wa chakula chenye sumu kuvu. Chakula chenye sumu kuvu kinachangia kupata magonjwa hayo .

Sumu kuvu ni aina ya sumu inayopatikana sana katika chakula inayotokana na uvunaji wa chakula, uhifadhi na utumiaji wake.
Ulaji wa chakula chenye sumu kuvu unachangia ugonjwa wa saratani katika mwili wa binadamu.
Katika Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, vimeanzishwa vituo 230 vya kutolea huduma ya kukabiliana na magonjwa yasiyoambukiza ambavyo ni vya serikali na binafsi .

Hii inatokana na magonjwa haya katika kipindi cha hivi karibuni kuongoza kwa wagonjwa wa nje (OPDs) na wale wanaolazwa katika vituo hivyo na hospitali.

Magonjwa haya yasiyoambukiza yanaathiri rika zote katika jamii yaani watu wazima na watoto.

Matokeo ya malezi yasiyo mazuri na sahihi kwa watoto yanachangia watoto wengi kuwa na uzito mkubwa (over Weight).
Ulaji wa chakula cha mafuta mengi, sukari nyingi hasa kwenye chakula kama chocolate, burger,pipi, biskuti, chakula chenye wanga mwingi na kutokufanya mazoezi kwa watoto hao kuanzia nyumbani hadi shuleni, huchangia kuenea kwa maradhi hayo katika kundi la watoto.
Sambamba na hilo familia na malezi ya sasa yamekua tofauti kama zamani.
Asilimia kubwa ya watoto siku hizi hawafanyia mazoezi. Pia mtindo wao wa maisha yao kwenda shule na kurudi nyumbani kwa kutumia magari na vyombo vingine vya moto kama bajaji na pikipiki vinachangia kupata maradhi yasioambukiza.

**MLO SAHIHI KWA WATOTO.**
Mlo sahihi ni mchanganyiko sahihi wa makundi muhimu ya chakula kama protini, wanga, vitamin, madini na mafuta.
Mtoto anatakiwa kula chakula cha wanga cha kutosha kama ugali, ndizi, wali, ngano,uwele.
Chakula cha protini kama vile samaki, mayai, maziwa, nyama, kunde, maharage, mbaazi, mboga za majani,dagaa,kumbikumbi na senene.
Chakula cha vitamin ni pamoja na matunda,mboga za majani, mboga za kijani, nyama,parachichi na korosho.
Hivyo wazazi wanatakiwa kufuata ratiba ya kuwapa watoto chakula na wahakikishe mchanganyiko huo wa chakula unakua wa kiwango na kuwapa watoto kwa muda sahihi.
Inaelezwa katika kipindi cha hivi karibuni magonjwa yanayoongoza kwa top 10 kwa watoto wadogo ni magonjwa ya mfumo wa njia ya hewa na shinikizo la damu. Vilevile magonjwa mengine ni kama kuharisha, malaria, shinikizo la damu,UKIMWI, homa ya tumbo, homa ya mapafu, kisukari na ajali.

**MIKAKATI KUDHIBITI MAGONJWA YASIYOAMBUKIZWA**
Mikakati hii imegawanyika katika maeneo matatu. Kwanza kuzuia magojwa yasiyoambukiza, mikakati kwa ajili ya kuwatambua waliopata ili wasije kuangukia katika dalili mbaya na mikakati kwa wale wenye matatizo.
Mikakati ya Kuzuia watu wasipate magojwa yasiyoambukiza. Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kupitia Idara ya Huduma za Afya katika Jamii imeweka mikakati ifuatayo;

**Elimu ya afya kwa umma.**

➤ Elimu hii inatolewa katika maeneo mbalimbali ili kuhakikisha wananchi wanaipata.
Mfano kuhakikisha kila kituo cha afya cha serikali au binafsi kila siku asubuhi watoa huduma za afya kwa jamii wanatoa elimu juu ya magonjwa mbalimbali ikiwemo na haya yasiyoambukiza kabla wagonjwa hao hawajaanza kupata matibabu.

Hii inafanywa katika makundi nakwa mtu mmoj mmoja anapoingia katika vituo hivi au kumuona daktari.
Pia Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, imeweka mikakati wa kutoa elimu kwa ugonjwa mmoja usioambukiza katika wiki au kila mwezi.

➤ Halmashauri pia imeweka utaratibu wa kutembelea jamii kwenye maeneo ya mbali yasiyofikiwa.

Njia inayotumika ni kuweka kambi maalumu ili kuhamasisha wananchi wamabadilisha chakula hasa kwa wale ambao tayari wameshapata madhara.

Pia kuchukua hatua za kuwasaidia wale ambao wameshapata maambukizi kwa kuhakikisha wanahudumiwa kwa kutumia vifaa vya kutosha pamoja na dawa.

# MAADHIMISHO YA WIKI YA TATHIMINI YA UTOAJI MIKOPO KWA WANAWAKE VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU












# JIJI LA DAR ES SALAM LATOA MKOPO BILIONI MBILI (2) KWA WANAWAKE VIJANA NA WATU WENYE ULEMAVU.

Na Amanzi Kimonjo

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Amos Makalla leo tarehe 02 disemba 2021 ameudhuria maadhimisho ya wiki ya tathimini ya utoaji mkopo kwa wanawake,vijana na walemavu katika viwanja vya Mnazi Mmoja vilivyopo Jijini Dar es salaam,Mkopo ambao ni utekelezaji wa agizo la serikali ya jamuhuri ya muungano wa Tanzania kuwa kila Halmashauri itoe asilimia 10 ya mapato ya ndani kama mikopo kwa vijana ,walemavu na wanawake .

Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam imekuwa ikitekeleza agizo la serikali la kuwezesha wananchi kiuchumi kwa kupitia makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ni kwa miaka mitatu sasa Halmashauri ya Jiji la imekuwa ikitekeleza agizo hilo na kuunga mkono juhudi za Rais wa Jamuhuri ya muungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan katika kujenga Tanzania imara na yenye maendeleo.

Vile vile,Mkurugenzi wa Halmashauri wa Jiji la Dar es salaam wakati anasoma risala mbele ya mgeni rasimi amesema "Hadi kufikia Juni, 2021 Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam imefanikiwa kutoa kiasi cha shilingi Bilioni 16.2 kutoka katika mapato ya ndani bilioni 12 na kutoka marejesho ni Bilioni 3.8, fedha hizi zimetolewa kwa vikundi 16165 ambapo wanawake ni 9970 vikundi vya vijana ni 536 na watu wenye ulemavu ni 835".

Kufuatia utoaji wa mikopo hiyo urejeshwaji kutoka katika makundi hayo Halmashauri imefanikiwa kukusanya kiasi cha shilingi Bilioni 3.8 ambapo wanawake ni kiasi cha shilingi Bilioni 1.1, vijana wamerejesha shilingi Milioni 788 sambamba na watu wenye ulemavu wamerejesha shilingi Milioni 267.

Sambamba na hilo pia Mhe. Makala ameweza kutoa hundi ambayo itawezesha vikundi vipya vitakavyo pewa mkopo pia akaendelea kusema "ninatoa hundi ya bilioni 2 kwa vikundi 97 wanawake 46 vijana vikundi 43 na walemavu vikundi 8 jumla ya Bilioni 2 na elfu ishirini na saba (27) haya yote yanafanyika ni kwa usimamizi mkubwa wa Rais wetu wa Jamuhuri ya Muuungano wa Tanzania Mhe. Samia Suluhu Hassan anatusimamia na kutuongoza wakurugenzi,wakuu wa mkoa,wakuu wa wilaya,wabunge na madiwani hizi pesa zitolewe kwa wanawake walemavu na vijana."

Aidha, Mhe Makalla ambaye ni mgeni rasimi katika maadhimisho hayo amesema "naagiza manispaa zote kuiga mfano wa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam katika kutoa mikopo isiyo na riba na yenye mashariti nafuu kwa wananchi na kuwakwamua kiuchumi wananchi hao pia mikopo mnayopewa muirejeshe kwa haraka na wengine nao wapate".

Nae Mkuu wa Wilaya ya Ilala ya Ilala Mhe.Ng'ilabuzu Ndatwa Ludigija amesema "kwanza natoa shukrani zangu za dhati kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam kwa kukubali mwaliko huu kuja kaungana na wajasiriamali hawa wanaopokea mkopo wa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam kama sehemu ya utekelezaji wa ilani ya chama cha mapinduzi na naona mafanikio ya hawa wajasiriamali tunaona kuna hadi kosta za hapa zilizotokana na mikopo hii na zinamilikiwa na wanachi waliopewa mkopo na kuzitumia wenyewe".

Maaadhimisho hayo pia yaliudhuriwa na wabunge wa majimbo yote matatu yaliopo katika Jiji la Dar es salaam ikiwa ni Mhe.Bona Kamori Jimbo la Segerea,Mhe.Jerry Silaa Jimbo la Ukonga na Mhe. Azan Zungu Jimbo la Ilala Pamoja na wakuu wa idara na madiwani wa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam.

# #Usikilizaji wa Kero za Wananchi ndani ya Wilaya ya Ilala










# HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM


*Jarida hili hutolewa na;*

Kitengo cha Habari, Uhusiano na Mawasiliano

S.L.P 20950, DAR ES SALAAM, TANZANIA

OFISI YA MKURUGENZI
1 MTAA WA MISSION
SIMU: 2128800
2128805
WEBSITE: www.dcc.go.tz
EMAIL:administration@dcc.go.tz